

USIMAMIAJI WA MAADILI YA UTENDAJI KAZI KATIKA UTUMISHI WA UMMA.

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

1.0 UTANGULIZI

Utendaji wa kazi katika utumishi wa umma huongozwa na maadili ya kazi ambayo yametayarishwa na serikali kwa ajili ya watumishi wote wa umma. Watumishi wote wa umma wanao wajibu wa kufanya kazi kwa kufuata maadili hayo. Ili suala hili liweze kutekelezwa ipasavyo na watumishi wote wa umma, mamlaka za nidhamu katika utumishi wa umma zina wajibu wa kutoa elimu juu ya maadili na kuwapatia watumishi wao mwongozo wa maadili ya kazi katika utumishi wa umma na kuwasainisha watumishi makubaliano ya kuzingatia maadili hayo. Endapo mtumishi wa umma atatenda kazi zake kinyume cha maadili ya kazi atakuwa ametenda kosa la kinidhamu na itabidi achukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma. Taratibu za kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi waliokiuka maadili ya kazi zao zinapaswa kuchukuliwa kwa haki na usawa na Mamlaka zao za nidhamu. Uzingatiaji mzuri wa maadili ya kazi katika sehemu za kazi hujenga maelewano miongoni mwa watumishi na husaidia utoaji mzuri wa huduma kwa wananchi.

2.0 MAADILI

Utekelezaji wa maadili ya kazi una uhusiano mkubwa na uchukuaji wa hatua za kinidhamu kwa watumishi waliokiuka maadili ya kazi zao. Hii ina maana kwamba mtumishi wa umma akitenda kinyume na maadili ya kazi yake huchukuliwa hatua za kinidhamu na mamlaka yake ya nidhamu. Hivyo, ili kuweza kutekeleza suala la kinidhamu kwa haki na usawa katika utumishi wa umma mamlaka za nidhamu hazina budi kutekeleza masuala ya kinidhamu kwa kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na kanuni zake za mwaka 2003. Aidha, ili mamlaka za nidhamu ziweze kutekeleza vizuri masuala ya kinidhamu hazina budi pia kutoa elimu juu ya maadili ya utumishi wa umma na kusimamia hatua za utekelezaji wa maadili hayo katika sehemu zao za kazi. Hatua za utekelezaji wa maadili hayo ni kama zifuatavyo:

21. Kuwapatia watumishi mwongozo wa maadili ya utumishi wa umma (Kanuni Na.66(1). Katika hatua hii mamlaka za nidhamu zinapaswa kuhakikisha kuwa kila mtumishi amepatiwa nakala ya mwongozo wa maadili kwa lengo la kupata nafasi ya kusoma na kuelewa yale ambayo yameelekezwa katika mwongozo huo. Mwongozo wa maadili ya watumishi wa umma pia unapatikana katika jedwali la tatu la kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2003.

2.2 Kumsainisha mtumishi makubaliano ya kuzingatia maadili ya kazi(kanuni Na.66 (2) kwa kutumia Fomu za makubaliano ya kuzingatia maadili ya kazi. Fomu hii itajazwa na mtumishi na kuthibitishwa na mwajiri

2.3 Kuchukua hatua dhidi ya mtumishi anayekiuka maadili ya kazi(kanuni Na.67). Katika kutekeleza hatua hii mamlaka za nidhamu zinapaswa kutenda kwa kufuata haki, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na sheria zingine za nchi.

3.0 HITIMISHO

Ili haki na usawa viweze kutendeka katika utumishi wa umma mamlaka zote za nidhamu zinapashwa kutekeleza masuala yote ya nidhamu kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa umma Na 8 ya mwaka 2002 na kanuni zake za mwaka 2003.

Ndugu msomaji, iwapo una maswali au maoni tafadhali wasiliana nasi kwa anwani ifuatayo:

Katibu,

Ofisi ya Rais

Tume ya Utumishi wa Umma

Jengo la Acasia, Mtaa wa Samora

S.L.P 9143

Dar es Salaam.

Simu: +255(22) 2126811/4, 216260 Faksi: +255(22) 2114158